LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: +255 22 2773048, +255 22 2773038, 0764 418773, 0787 343841 Fax: +255 22 2773037,
E-mail: lhrc@humanrights.or.tz, Website www.humanrights.or.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MWENENDO WA MCHAKATO WA UTUNGAJI WA KATIBA MPYA TANZANIA

Tarehe 7 Agosti 2014

Ndugu wanahabari,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari kimeendelea kufuatilia kwa umakini na ukaribu mchakato wa Katiba Mpya ikiwemo hatua ya sasa ya Bunge Maalum la Katiba lililoanza tena tarehe 5 Agosti 2014 mjini Dodoma bila ya baadhi ya wajumbe wa Bunge hilo hasa wale wa kutoka kundi linalojiita UKAWA (Umoja wa Katiba ya Wananchi) ambao walijiengua kwenye vikao vya Bunge hilo kwa madai ya kutoafiki mwenendo wa vikao vya Bunge la Katiba. Kwa nyakati tofauti tumeendelea na juhudi za kuona uwezekano wa usuluhishi wa mgogoro huu ili kuhakikisha pande zote zinaendelea kukamilisha hatua za kuandika Katiba itakayowafaa wananchi wa Tanzania bila kujali itikadi zao.

Ndugu wanahabari,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tumepata mshtuko mkubwa na kusikitishwa na kauli za baadhi ya viongozi wa Serikali pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Bunge Maalum kuhusiana na mchakato wa Katiba nchini Tanzania. Kauli hizo na matamko hayo yanaashiria mwelekeo mbaya sana wa kukiuka misingi ya demokrasia na utawala wa sheria, kuminya uhuru wa vyombo vya habari na haki ya kutoa maoni; na pia kwa kiwango kikubwa sana yanakiuka haki za binadamu nchini Tanzania kama zinavyolindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Hususan Ibara ya 18 na 21(2).

Ndugu wanahabari,

Kwa kuwakumbusha ibara hizi za Katiba ya Tanzania zinasomeka kama ifuatavyo:

Ibara ya 18 inasomeka:

Kila Mtu

(a) Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;

Board of Directors:
Prof. Geoffrey Mmari Chairperson, Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Dr. Helen Kijo-Bisimba, Mr. Francis Stolla (Adv),
Ms. Athanasia Soka (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya

(b) *Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari habari bila ya kujali mipaka ya nchi*

(c) *Anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na*

(d) *Anayoa haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii*

Pia ibara ya 21(2) inasomeka;

(2) *Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa.*

Yafuatayo ni baadhi ya matamko hayo:-

1. Agizo la kupigwa marufuku Mijadala ya Katiba nje ya Bunge la Katiba:

Mnamo tarehe 4 Agosti 2014 Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Dr. Rehema Nchimbi amekaririwa akitoa tamko kwa umma kupiga marufuku makongamano na mikutano ya hadhara yenye lengo la kujadili masuala ya Katiba na Rasimu ya Katiba nje ya Bunge la Katiba na maeneo yote ya mkoa wa Dodoma kwa madai ya kuepuka kuwachanganya wajumbe wa Bunge la Katiba. Katazo hili ni kinyume kabisa na Ibara ya 18 na ya 21(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zinatoa haki kwa kila mwananchi kupata na kutoa habari, pia uhuru wa kushiriki uamuzi katika masuala yote yanayomhusu na kuathiri maisha yake na ya jamii yake. Aidha tunatambua kuwa Kila mwananchi anayo haki ya kujadili, kuuliza, kuhabarisha au kuzungumza kuhusu katiba. Tumeshuhudia midahalo huru ya umma ikiwa na manufaa makubwa kwa kuwakumbusha wananchi mambo muhimu katika rasimu ya katiba na hivyo kuongeza ushiriki mkamilifu wa wananchi katika mchakato wa kujipatia katiba yao.

2. Zuio kwa vyombo vya habari kutangaza mijadala ya Katiba

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tumesikitishwa na pia tunapinga vikali mapendekezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Bunge la Katiba Mh. Samwel Sitta mnamo tarehe 5 Agosti 2014 yenye dhana ya kukerwa na midahalo ya katiba inayoendelea. Tunapinga maelekezo yake kwa Serikali ya Tanzania kupiga marufuku vyombo vya habari kutangaza midahalo inayohusu katiba na Rasimu ya Pili ya Katiba. Matamshi hayo yaliyotolewa ndani ya Bunge la Katiba ni kinyume na ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano aliyoapa kuilinda na kuitetea. Matamko kama haya yana lengo la kuwazuia watanzania kupata habari na taarifa juu ya mwenendo wa uboreshaji wa maoni yao yaliyomo kwenye rasimu ya pili ya Katiba na kujua hatma ya Mchakato wa Katiba. Ikumbukwe kuwa Serikali ilishaifuta hata tovuti ya iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na

Board of Directors:
Prof. Geoffrey Mmari Chairperson, Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Dr. Helen Kijo-Bisimba, Mr. Francis Stolla (Adv),
Ms. Athanasia Soka (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya

kuwafanya wananchi wakose taarifa zote muhimu zilizokuwa zimetolewa na Tume hiyo. Tabia hii ya kuwafunga midomo watoa habari na kuwafumba macho wananchi ili wasiweze kushiriki kikamilifu katika kuandika katiba yao haikubaliki kamwe na ni kinyume na misingi ya demokrasia.

3. Majaribio ya kuzuia Waliokua wajumbe wa Tume ya Katiba Kuelimisha Wananchi juu ya maudhui ya Rasimu ya Pili ya katiba

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tunalaani vikali hatua zilizopendekezwa na Wajumbe wa Bunge Maalum za kutaka kuwazuia waliokua wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuzungumzia mchakato wa Katiba. Mapendekezo hayo ni mabaya kwa kuwa yatawazuia waliokua wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kutumia haki yao kama raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika mijadala ya kuwaelimisha wananchi wa Tanzania kuhusu maudhui ya Rasimu ya Pili ya Katiba. Pendekezo lao hilo linakiuka Ibara ya 18 na 21 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kituo kinaona huu kuwa ni upotoshaji na mwendelezo wa makosa makubwa kama yaliyokwisha kufanyika awali ya kuvunjwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba tarehe 19 Machi 2014 kwa gazeti la Serikali na. 81 chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kabla ya mchakato wa Katiba kufikia hatma yake.

Wajumbe wa Tume ndiyo waliokuwa na wajibu wa kukumbusha na kutoa ufafanuzi kwa Bunge la Katiba na wananchi juu ya hoja yoyote inayohusu mchakato wa katiba na maudhui ya Rasimu ya pili ya Katiba kwa kuzingatia ukweli kwamba wao ndio walipewa mamlaka chini ya sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83 kukusanya na kuratibu maoni ya wananchi na kuiunda Rasimu ya Katiba. Kutokana na kukosekana kwa Tume hiyo, baadhi ya wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba wamejisahau na kuzungumza mambo ambayo hayahusiani kabisa na Rasimu ya Pili ya Katiba huku wengine wao wakitumia lugha za matusi na kejeli dhidi ya Tume.

4. Mabadiliko holela ya Kanuni za Bunge la Katiba

Kituo kinaendelea kukemea na kusisitiza kuheshimiwa kwa kanuni za Bunge la Katiba. Mabadiliko ambayo yanafanywa katika kanuni kwa manufaa ya kundi mojawapo katika Bunge Maalum yatapelekea kupatikana kwa katiba ambayo haina ridhaa ya kisiasa na wananchi kiujumla. Ni vema mjadala wa katiba ukajengwa katika kuleta Muafaka wa pamoja na kuheshimu makundi yote katika jamii ikiwemo makundi ya "wachache".

Board of Directors:
Prof. Geoffrey Mmari Chairperson, Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Dr. Helen Kijo-Bisimba, Mr. Francis Stolla (Adv),
Ms. Athanasia Soka (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya

Moja ya mabadiliko ni ya kuacha kuhitimisha mjadala wa sura mbili zilizojadiliwa kwa kupiga kura nakuendela na sura zingine zote zilizosalia. Iwapo hapajakua na maridhiano na muafaka wa sura hizi ambazo zinagusa muundo wa muungano ambao ndio kitovu cha katiba kwa sasa majadiliano yaliyopo yatakuwa yanabebwa na msingi upi? Tunaona huu ni upotezaji wa muda.

Ndugu wanahabari,

Kwa kuhitimisha, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tunalitaka Bunge la Katiba pamoja na Serikali kuheshimu uhuru wa kutoa maoni na kupokea habari kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ni vema wadau wote wakaepuka kutoa kauli ambazo zitakua chanzo cha kuzorotesha umoja na amani kwa taifa la Tanzania. Wananchi wapewe uhuru wa kujadili hatma ya Taifa lao kupitia mchakato wa katiba mpya, hii ni pamoja na wajumbe wa Bunge la Katiba kuheshimu mawazo ya wananchi yaliyomo ndani ya Rasimu ya pili ya Katiba. Tunapendekeza Bunge hilo la Katiba kusitisha mijadala ya sura zilizosalia na kufanya kila liwezekanalo kumaliza mgogoro kati yao ili majadaliano yakiendela kuwepo na uhakika wa kufikia kupiga kura na mapendekeo ya katiba mpya yawe na uhalalai wa kisheria na kisiasa.

Asanteni kwa kunisikiliza,

.....

Dkt. Helen Kijo-Bisimba
Mkurugenzi Mtendaji

Board of Directors:
Prof. Geoffrey Mmari Chairperson, Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Dr. Helen Kijo-Bisimba, Mr. Francis Stolla (Adv), Ms. Athanasia Soka (Adv), Ms. Maria Sarungi Tschai, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya